



## TAARIFA KWA UMMA

### MSAMAHA WA ADA YA UWASILISHAJI WA NYARAKA ZA KAMPUNI ZILIZOSAJILIWA KABLA YA MWAKA 2018

**Dar es Salaam-4 Juni, 2024**

Msajili wa Kampuni anapenda kuwafahamisha Wadau na Umma kwa ujumla kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe Dkt. Ashatu Kijaji, ametoa Notisi ya Msamaha wa asilimia hamsini (50%) ya ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda iliyotolewa katika Tangazo la Serikali Na. 410 la tarehe 24 Mei, 2024 na itatumika kwa kipindi cha miezi kumi na mbili tangu kuchapishwa kwake.

Waziri ametoa Notisi hiyo kwa kuzingatia kifungu cha 452A cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 kinachotoa Mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara kutoa msamaha wa ulipaji wa ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda. Notisi hii imetolewa kwa lengo la kuwezesha uhuishaji wa taarifa za kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018 kwenye mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandaoni (Online Registration System)

Kufuatia notisi hiyo, Msajili wa Kampuni anawataarifu kuwa msamaha wa asilimia hamsini (50%) unatolewa kwa ada ya ucheleweshaji wa nyaraka (late filing fee) kwa Kampuni zenye sifa zifuatazo;

- Kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018 ambazo taarifa zake hazijahuishwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao,
- Maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni yaliyopo kwenye Mfumo wa usajili wa kampuni kwa njia ya Mtandao kabla ya tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii,
- Maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao yatakayopokelewa kwenye Mtandao ndani ya muda wa Notisi hii,

Aidha, ifahamike kwamba maombi yaliyokwisha wasilishwa kwenye Mfumo na kupitishwa na Msajili au Msajili kuingia makubaliano yoyote na Kampuni husika ya jinsi ya kufanya malipo husika kabla ya tarehe ya Notisi hayatahusika na msamaha huu.

Msajili anazielekeza Kampuni zote zinazohusika na Msamaha huu kuwasilisha taarifa zao kwa Msajili kupitia mfumo wa ORS ndani ya muda ulioelekezwa ili kunufaika na msamaha huo.

Imetolewa na;  
**Kitengo cha Uhusiano**